# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# MWONGOZO WA KUWAREJESHA SHULENI WANAFUNZI WALIOKATIZA MASOMO KATIKA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI KWA SABABU MBALIMBALI

JUNI, 2022

## 1.0. UTANGULIZI

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloja (WyEST) imeridhia mikataba, matamko, Sera na Sheria mbalimbali za kimataifa na kikanda yanayolenga utoaji wa haki ya elimu kwa wote bila ubaguzi. Katika muktadha huo, Dira ya elimu inalenga kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali imeandaa **Mwongozo wa Kuwarejesha Shuleni Wanafunzi Waliokatiza Masomo katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa Sababu Mbalimbali** ili waweze kukamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika.

## 2.0 MALENGO YA MWONGOZO

### 2.1 Lengo Kuu

Lengo la jumla la mwongozo huu ni kutoa maelekezo yatakayowezesha urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo ili waweze kukamilisha mzunguko wa masomo yao katika mfumo rasmi.

### 2.2 Malengo Mahsusi

i. Kuwezesha urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo katika shule za msingi na Sekondari;
ii. Kushirikisha wadau kuhusu wajibu wao katika kuwarejesha wanafunzi waliokatiza masomo; na
iii. Kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo.

## 3.0 WALENGWA/WANUFAIKA WA MWONGOZO

Walengwa wakuu wa Mwongozo huu ni WyEST pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi zisizo za kiserikali, watu binafsi, jamii, wadau wanaojishughulisha na utoaji wa elimu ya msingi na sekondari, wazazi/walezi pamoja na wanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari waliokatiza masomo. Mwongozo huu unahusu shule zote za Serikali na zisizo za Serikali Tanzania Bara. Aidha, Mwongozo hautahusika kuwarejesha shuleni wanafunzi

waliokatiza masomo kwa sababu ya utovu wa nidhamu unaosababishwa na makosa ya jinai na wanafunzi waliofukuzwa shule kwa sababu za kuhatarisha amani.

## 4.0 UREJESHWAJI WA MWANAFUNZI ALIYEKATIZA MASOMO KWA SABABU MBALIMBALI

Urejeshwaji shuleni wanafunzi waliokatiza masomo utategemea sababu za mwanafunzi husika kukatiza masomo. Hivyo, wanafunzi wa makundi yafuatayo watapaswa kukamilisha na kuzingatia taratibu za urejeshwaji wao shuleni kama inavyoelezwa hapa chini:

### 4.1 Ujauzito

#### 4.1.1 Taratibu za Kumrejesha Shuleni Mwanafunzi Aliyekatiza Masomo Kutokana na Ujauzito

i. Kurejea shuleni ndani ya miaka miwili baada ya kukatiza masomo;
ii. Uongozi wa Shule uitishe kikao cha pamoja baina ya Mzazi/Mlezi na Kamati/Bodi ya Shule kujadili namna ya kumsaidia mwanafunzi husika;
iii. Wazazi/walezi waridhie kwa maandishi kuwa watamhudumia mtoto wao pamoja na mtoto aliyezaliwa kwa kuwapa msaada na huduma stahiki wakati mwanafunzi akiendelea na masomo;
iv. Mwanafunzi arejee shuleni mwanzo wa mwaka mpya wa masomo katika darasa alilokatiza masomo;
v. Mwanafunzi aruhusiwe kuchagua kurudi katika shule ya mwanzo au kuhamia shule nyingine kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Ikitokea akapata ujauzito tena hataruhusiwa kuendelea na masomo katika Mfumo Rasmi wa Elimu;
vi. Kupewa huduma ya ushauri na unasihi;
vii. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi aliyerejea shuleni baada ya kujifungua kwenda shuleni na mtoto wake; na
viii. Upimaji wa mwanafunzi ili kubaini hali ya ujauzito utafanyika kwa hiari ya mwanafunzi husika au kwa sababu za kimatibabu kwa faida ya mwanafunzi husika, ambapo utaratibu huu wa hiari utahusisha mwanafunzi yeyote anayeendelea na masomo au yule anayerejea shuleni baada ya kukatiza masomo kutokana na ujauzito.

## 4.2 Ulemavu

### 4.2.1 Taratibu za Kumrejesha Shuleni Mwanafunzi Mwenye Ulemavu

i. Kurejea shuleni katika kipindi kisichozidi miaka minne baada ya kukatiza masomo na kuthibitika kuwa ni mwenye ulemavu;
ii. Endapo baada ya miaka miwili itathibitika kwamba mwanafunzi mwenye ulemavu bado ana changamoto ya kurejea shuleni ataongezewa muda ili kumpa fursa ya kutatua changamoto husika na kurejea shuleni ndani ya miaka miwili;
iii. Uongozi wa Shule uitishe kikao cha pamoja baina ya Mzazi/Mlezi na Kamati/Bodi ya Shule kujadili namna ya kumsaidia mwanafunzi husika;
iv. Wazazi/walezi kwa kushirikiana na Mkuu wa Shule pamoja na Afisa Elimu Maalumu katika Halmashauri husika watafute shule jumuishi/maalum (bweni kama itahitajika) yenye uwezo wa kumpatia mwanafunzi huduma stahiki;
v. Kurejea shuleni mwanzo wa mwaka mpya wa masomo katika darasa alilokatiza masomo;
vi. Kuruhusiwa kuchagua kurudi katika shule ya mwanzo au kuhamia shule nyingine;
vii. Kupewa nafasi katika shule ya bweni/dahalia iwapo italazimika;
viii. Uongozi wa shule, wazazi/walezi kwa kushirikiana na Serikali kupitia Halmashauri husika imwezeshe mwanafunzi kupata vifaa saidizi kulingana na mahitaji; na
ix. Kupewa huduma ya ushauri na unasihi.

## 4.3 Sababu Nyinginezo

### 4.3.1 Taratibu za Kuwarejesha Wanafunzi Waliokatiza Masomo kwa Sababu Nyinginezo

Kundi hili linajumuisha wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu nyinginezo ikijumuisha umaskini, utoro, watoto kuwa walezi wa familia zao, ajira za ututoni, kuishi katika mazingira magumu, umbali kutoka nyumbani hadi shuleni, kuishi na mzazi/mlezi mmoja pamoja na kutowajibika kwa wazazi. Zifuatazo ni taratibu za kufuatwa ili kuwarejesha shuleni wanafunzi husika:

i. Mwanafunzi atatakiwa kurejea shuleni ndani ya miaka miwili tangu kukatiza masomo;
ii. Uongozi wa Shule uitishe kikao cha pamoja baina ya Mzazi/Mlezi na Kamati/Bodi ya Shule kujadili namna ya kumsaidia mwanafunzi husika;
iii. Mwanafunzi aruhusiwe kuchagua kurudi katika shule ya mwanzo au kuhamia shule nyingine;

iv. Mwanafunzi apewe huduma ya ushauri na unasihi;
v. Mwanafunzi arejee shuleni mwanzo wa mwaka mpya wa masomo katika darasa alilokatiza masomo;
vi. Uongozi wa Shule uitishe kikao cha pamoja baina ya Mzazi/Mlezi na Kamati/Bodi ya Shule ili kujadili namna ya kumpatia mwanafunzi msaada stahiki; na
vii. Uongozi wa shule, wazazi/walezi kwa kushirikiana na Serikali kupitia Halmashauri imtafutie mwanafunzi husika shule iliyo karibu na makazi iwapo kuna ulazima.

## 5.0 WAJIBU WA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

### 5.1 Wajibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

i. Kusimamia Sera, Sheria na kutoa miongozo inayohusu urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo;
ii. Kutoa elimu na msaada wa kitaalamu juu ya utekelezaji wa mwongozo;
iii. Kushirikiana na wadau kuwezesha utekelezaji wa mwongozo; na
iv. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mwongozo.

#### 5.1.1 Wajibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

i. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo; na
ii. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mwongozo.

#### 5.1.2 Wajibu wa Afisa Elimu wa Mkoa

i. Kuratibu uandaaji wa takwimu husika na kutoa taarifa;
ii. Kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya Msingi na Sekondari wanaandikishwa/kupangwa katika shule zilizopo jirani na maeneo wanayoishi kadri inavyowezekana;
iii. Kushirikiana na wadau kurejesha wanafunzi shuleni;
iv. Kuandaa na kusimamia mikakati ya kuwalinda wanafunzi waliorejeshwa shuleni ili waweze kuendelea na masomo; na
v. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya wanafunzi waliorejeshwa shuleni na kuiwasilisha OR – TAMISEMI.

#### 5.1.3 Wajibu wa Afisa Elimu Msingi/Sekondari

i. Kutoa elimu kuhusu urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo;

ii. Kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya Msingi na Sekondari wanapangwa katika shule zilizopo jirani na maeneo wanayoishi;
iii. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata vifaa vya kielimu na saidizi kulingana na mahitaji yao;
iv. Kuratibu utekelezaji wa mwongozo huu;
v. Kusimamia utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi shuleni;
vi. Kufuatilia na kufanya tathmini ya urejeshwaji wa wanafunzi shuleni; na
vii. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya wanafunzi waliorejeshwa shuleni na kuiwasilisha katika ngazi ya Mkoa.

### 5.1.4 Wajibu wa Afisa Elimu Kata

i. Kutoa elimu kuhusu urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo katika ngazi ya Kata;
ii. Kuhakikisha wanafunzi wa elimu ya Msingi na Sekondari wanapangwa katika shule zilizopo jirani na maeneo wanayoishi;
iii. Kuratibu upatikanaji vifaa vya kielimu na saidizi kulingana na mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
iv. Kuratibu utekelezaji wa mwongozo huu;
v. Kusimamia utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi shuleni;
vi. Kufuatilia na kufanya tathmini ya urejeshwaji wa wanafunzi shuleni; na
vii. Kuandaa taarifa ya maendeleo ya wanafunzi waliorejeshwa shuleni na kuiwasilisha katika ngazi ya Halmashauri.

### 5.1.5. Wajibu wa Jamii

i. Kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanafunzi;
ii. Kubadilishana uzoefu na elimu kuhusu ulinzi wa watoto dhidi ya mimba na ndoa za utotoni, matumizi ya madawa ya kulevya, ajira za utotoni pamoja na madhara yatokanayo na vitendo hivyo; na
iii. Kushirikiana na shule kuhakikisha wanafunzi wote shuleni wanashiriki masomo kikamilifu.

### 5.1.6. Wajibu wa Bodi/Kamati ya Shule

i. Kushirikiana na uongozi wa shule pamoja na wazazi/walezi ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi aliyekatiza masomo anarejea shuleni na kupata huduma stahiki;
ii. Kuhakikisha kuwa huduma ya ushauri na unasihi inatolewa shuleni; na
iii. Kushiriki katika ufuatiliaji na tathmini ya urejeshwaji wa wanafunzi shuleni.

### 5.1.7. Wajibu wa Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu

i. Kuhakikisha wanafunzi waliorejeshwa shuleni wanahudhuria na kujifunza kikamilifu;
ii. Kuandaa mazingira wezeshi na rafiki kwa wanafunzi waliorejeshwa shuleni;
iii. Kumsaidia mwanafunzi aliyekatiza masomo kuhamia shule nyingine ikiwa hayuko tayari kuendelea na masomo katika shule ya awali;
iv. Kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wakiwemo wanaorejea shuleni baada ya kukatiza masomo wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za shule;
v. Kuhakikisha uwepo wa sanduku la maoni shuleni ili, pamoja na mambo mengine, kubaini changamoto zinazowakabili wanafunzi wanaorejea shuleni;
vi. Kuhakikisha kuwepo kwa huduma ya malezi, ushauri na unasihi shuleni; na
vii. Kutunza kumbukumbu za wanafunzi waliorejea shuleni na kuhakikisha kuwa usiri unazingatiwa.

### 5.1.8. Wajibu wa Mshauri na Mnasihi wa Wanafunzi

i. Kutoa huduma ya malezi, ushauri na unasihi kwa wanafunzi wote wakiwemo waliorejea shuleni baada ya kukatiza masomo;
ii. Kuwasaidia watoto kutambua haki na wajibu wao; na
iii. Kuwashauri wazazi/walezi kuhusu namna bora ya kuishi na mwanafunzi mwenye changamoto mbalimbali kabla na baada ya kurejea shuleni.

### 5.1.9. Wajibu wa Mzazi/Mlezi

i. Kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji ya msingi kwa mtoto aliyerejea shuleni;
ii. Kushiriki kikamilifu katika kuwarejesha watoto shuleni;
iii. Kufuatilia maendeleo ya watoto na kushiriki vikao vya shule;
iv. Kuhakikisha uwepo wa mazingira rafiki na salama kwa watoto;
v. Kuwaelimisha watoto kwa uwazi kuhusu changamoto mbalimbali zinazosababisha kukatiza masomo;

vi. Kumtafutia mwanafunzi shule atakayokuwa tayari kurejea kwa kushirikiana na uongozi wa shule; na
vii. Kuwashawishi na kuwatia moyo wanafunzi waliokatiza masomo ili warejee na kuendelea na masomo.

#### 5.1.10. Wajibu wa Mwanafunzi Anayerejea Shuleni

i. Kuzingatia masomo na kuepuka vitendo hatarishi vinavyoweza kusababisha mwanafunzi kukatiza masomo;
ii. Kuzingatia maadili mema pamoja na Sheria, Kanuni na Taratibu za shule; na
iii. Kutoa taarifa kuhusu vitendo vya udhalilishaji na unyanyapaa.

## 6.0. UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 6.1. Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utajikita katika kubaini ufanisi na changamoto za utekelezaji wa mwongozo huu. Taarifa zitakazokusanywa zitaandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau katika ngazi mbalimbali kwa hatua zaidi.

### 6.2. Tathmini

WyEST kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI itafanya tathmini ya utekelezaji wa mwongozo huu kila mwisho wa mwaka wa masomo.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**